Journal Homepage: -www.journalijar.com

INTERNATIONAL JOURNAL OF ADVANCED RESEARCH (IJAR)

ISSN NO. 2320-5407

Article DOI:10.21474/IJAR01/7979
DOI URL: http://dx.doi.org/10.21474/IJAR01/7979

*RESEARCH ARTICLE*

# UTATHIMINI WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA ZILIZOTEULIWA KUTAHINIWA KATIKA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA: MSTAHIKI MEYA (2009) NA KIGOGO (2016).

**Muthui Evelyn Kakivi and Esther Njoki Chomba**

……………………………………………………....……………………………………………………………….....

***Manuscript Info***

……………………….

***Manuscript History***
Received: 01 September 2018
Final Accepted: 03 October 2018
Published: November 2018

***Keywords:-***
Maudhui makuu; tamthilia teule, Uhalisia, kutahiniwa, jamii.

***Abstract***

………………………………………………………………………………..

Utafiti huu unalenga kutathmini uhalisia wa maudhui katika tamthilia zilizoteuliwa kitahiniwa katika shule za upili hususan tamthilia ya *mstahiki meya* (Arege, T. 2009) na *Kigogo* (Kea, P. 2016). Katika kuzisoma tamthilia hizi na kuzitathmini tamthilia hizi, ni kweli kuwa tamthilia hizi zina ukaribiano wa kimaudhui lakini je kazi hizi za tamthilia zilihahakisi uhalisia wa mambo katika jamii kipindi ambacho ziliteuliwa kutahiniwa? Hata hivyo mtafiti alijiuliza kuwa je, ni kigezo kipi kinatumiwa kuteuwa tamthilia hizi kuwa za kutahiniwa katika kipindi Fulani ilhali zafanana kimaudhui? Je ni hali halisi ya kimaisha katika jamii wakati wa kuteua kazi hizi? Ikiwa ni hivyo,mtafit anatarajia kuzichunguza tamthilia hizi ili kubainihali ya uhalisia wa kijamii wakati katika kpindi cha kuteuliwa tamthilia hizi ili kubaini ufaafu wake kwa wanafunzi ambao ni kiwakilishi cha jamii kwa wakati ule.Utafiti huu utatathmini maudhui katika tamthilia hizi na kuonyesha umuhimu wake kwa wanafunzi na uhalisia wake katika jamii katika kipindi cha kuteuliwa kwake.Tutauchanganua maudhui katika kazi hizi mbili mintaaarafu matukio na hali halisi za kijamii na kuzitathmini tukitumia nadharia ya uhalisia. Kwa kutumia msingi ya nadharia ya Uhalisia ili kufikia maamuzi ya kuwa ama maudhui ya tamthilia hizi yalifaa kwa kipindi cha kuteuliwa au la. Mtafiti atapendekeza njia mwafaka za kuteua kazi za fasihi za kutahiniwa kwa kurejelea matokeo ya utafiti wetu.Ili kufikia malengo yetu, utafiti utazichanganua tamthilia hizi kwa undani na tutarejelea matukio halisi kama yalivyoripotiwa katika vyombo vya habari, kusakura kwenye mitandao kubaini masuala halisi jamii kama vile ; maudhui ya kisiasa, mungawanyiko wa jamii kwa mipaka ya kijamii, chuki, ukabila miongoni mwa mambo mengine yanayoiadhiri jamii ya leo na kisha kutathmini kwa kutumia nadharia teule ya uhalisia ili kubaini iwapo tamthilia ambazo zinateuliwa zinalenga mambo yale kwa kuangalia maudhui makuu ya tamthilia ya *Mstahiki Meya(2009)*na *Kigogo(2016)*.Ni bayana kwamba mengi ya kuhusu maudhui yamefanywa katika tamthilia hizi hasa ikichukuliwa kwamba ni kazi ambazo zimetahiniwa katika shule za shule za upili katika vipindi tofauti. Hata hiyo utafiti huu unaegea zaidi kwa maudhui makuu ya kazi hizi ,kuyatathimini na na kuyaoanisha na mambo halisi katika jamii katika vipindi hivi vya utahini lengo kuu likiwa kuchunguza uhalisia wa maudhui makuu katika jamii na umuhimu wake kwa



**Corresponding Author:- Esther Njoki Chomba**

wanafunzi katika vipindi vile. Utafiti huu una sehemu tatu: sura ya kwanza inahusisha : suala la utafiti , maswali ya utafiti,malengo ya utafiti, mihili ya nadharia, sababu za kuchagua mada , upeo na mipaka na uteuzi wa data na uwasilishaji hata. Sura ya pili itashughulikia historia fupi ya waandishi wa tamthilia za *Mstahiki Meya* (2009)na *kigogo(2016)*, udurusu wa maandishi ya watafiti wengine ili kupata maoni yao kuujenga utafiti huu.Sura ya tatu itahusiana na mbinu za utafiti pamoja na zile za uchanganuzi wa data. Katika kukusanya data, utafiti huu utatumia mbinu ya kusoma makala maktabani na kusakura katika mitandao.sura ya nne ni sehemu ya uchanganuzi wa data iliyokusanywa kutoka kwa tamthilia teule na majibu ya hojaji za walimu na wanafunzi.sura ya tano ni ya muhutasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo.

*Copy Right, IJAR, 2018,. All rights reserved.*

**……………………………………………………………………………………………………………………**

**UTANGULIZI:-**

Kulingana na M.Msokilie (1992)Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu ili kueleza tajriba mbalimbali za maisha ya wanajamii. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi inawasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikizano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Fasihi inawasilisha maudhui yenye mguso kwa wanajamii kupitia kwa lugha iliyojaaa mvuto.Hivyo kwa jumla fasihi ni kielelezo cha hisia za mwandishi juu ya mambo yanayomwathiri yeye au jamii nzima anamoishi akilenga kustarehesha au kufunza wasomaji wake.

Njogu na Chimera (1999) wanafafanua kuwa msanii ni zao la jamii na inajaribu kuwasilisha matukio ya jamii katika uhalisia wake. Msanii anachota maudhui yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka za kitamaduni, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kupitia kwa kazi za fasihi tunapata picha kamili ya jamii ya kisasa. Hakuna fasihi inayoibuka katika ombwe tupu. Kila fasihi ni zao halisi la jamii na inaonyesha kuwepo kwa jamii hiyo kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Maudhui ambayo Arege .T (2009) na Kea .P (2016) wanaibua ni tajriba yao kijamii zinaeleza ukweli kuhusu maisha ya jamii.

Ni kwa sababu hii basi utafiti unalenga kutahimini uhalisia wa maudhui makuuKwa vile fasihi ni zao la wakati na jinsi jamii inavyobadilika ndivyo kazi ya fasihi inavyobadilika ikiwemo tamthilia za Kiswahili zinaendelea kukua ili kukidhi mahitaji ya jamii inayopitia mabadiliko katika nyanja za kijamii, kisiasa, kielimu, kiuchumi na kiteknolojia. Ni kwa sababu hii ya mabadadiliko ya fasihi kutengemea wakati iliyotupa mwelekeo wa usuli wa mada yetu kutathimini maudhui ya tamthilia teule ambazo zimetahiniwa katika shule za upili kwa kipindi kati ya miaka ya 2013 na 2018 utafiti ukilenga kuwatumia wanafunzi wa kata ndogo ya nzambani kaunti ya kitui ambalo ndilo eneo la utafiti kama kiwakilishi cha jamii nzima ya Kenya kuangalia ufaafu wa maudhui makuu kwa jamii na uhalisia wake katika jamii ya sasa.

Tamthilia za kisasa kwanza, zinaibua uhalisia; taratibu za maisha kama vile siasa, ufisadi, ukoloni mamboleo, umaskini, n.k zinatazamwa kwa jicho la ukali na udhaifu wake unafichuliwa bila uoga. Haya ni masuala halisi ambayo ni wazi katika jamii ya leo na ambayo hata wanajamii wa elimu ya chini anaweza kuyatambua. Pili, wahusika wanahusishwa zaidi na hisia zao na masuala ya utu wao; wanaingiliana na jamii pana kwa kuendeleza maudhui halisi katika jamii. Vilevile, wahusika halisi wanatumiwa kinyume na wahusika wanyama waliotumiwa awali uhalisia wa wahusika unatokea kupitia kwa majina yao ambayo ni ya majazi au kinaya. Kwa vile tamthilia zinazoandikwa zinalenga uhalisia wa jamii utafiti utatathimini ufaafu na uhalisia wa maudhui katika jamii kwa kuangalia maudhui makuu katika tamthilia za *Mstahiki Meya(2009)*na *Kigogo(2016)* na zaidi kuchunguza Maudhui halisi katika jamii wakati wa kusomwa na kufunzwa kwa tamthilia hizi teule.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu fasihi ya Kiswahili haswa tamthilia. Suala la maudhui limeshughulikiwa kwa wingi japo kwa namna nyingi watafiti wa awali wameshughulikia uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia. Utafiti huu utatathimini maudhui makuu pekee katika tamthilia teule za *kigogo na Mstahiki Meya* kwa ya kutaka kujua iwapo kazi za kifasihi na haswa tamthilia zinazoteuliwa kufunzwa kufunzwa na kutahiniwa shuleni za upili zinaangazia hali halisi ya maudhui ya kijamii kwa vile kulingana na maelezo ya fasihi msanii hupitisha hisia juu ya mambo yanayomwathiri yeye au jamii nzima anamoishi akilenga kustarehesha au kufunza wasomaji wake.

Utafiti huu ulilenga kubainisha yafuatayo baada ya kusoma na kuchambua Maudhui makuu katika tamthilia teule *Mstahiki Meya(2009)* na *Kigogo (2016)* na kuchunguza uhalisia wa Maudhui hayo katika jamii wakati wa utahini wa tamthilia hizi kwa kuwahoji walimu na wanafunzi kama kiwaklilishi cha jamii nzima ambayo kupitia kipasa sauti cha utunzi wa Arege,T na Kea, p tunapata hali halisi ya mambo yanayomwathiri mwanajamii:

1.Kubaini ufaafu wa tamthilia za kutahiniwa kwa kuwahoji walimu na wanafunzi kama kielelezo cha jamii na kutumia nadharia ya uhalisia kuchunguza uhalisia wa maudhui makuu katika tamthilia za *Mstahiki Meya(2009)* na *Kigogo(2016)* kisha kuchunguza Maudhui makuu halisi katika jamii wakati wa utunzi kusomwa na kutahiniwa kwa kazi hiz za kifasihi.

**Udurusu wa maandishi.**

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu fasihi ya Kiswahili haswa tamthilia. Suala la maudhui limeshughulikiwa kwa wingi japo kwa namna tofautitofauti. Utafiti huu utatathimini maudhui makuu pekee katika tamthilia teule za *kigogo na Mstahiki Meya*.kwa lengo la kubaini Uhalisia na ufaafu wa Maudhui yake kwa jamii nzima kwa kuwahoji walimu na wanafunzi kama kielelezo cha jamii na kutumia nadharia ya uhalisia kuchunguza uhalisia wa Maudhui yale kwa kipindi hicho.

Chacha (1980) amehakiki ushairi wa Abdilatif katika kiwango cha maudhui, akizingatia Sauti ya Dhiki na utenzi wa Adamu na Hawa. Chacha (1980) alitumia mtazamo wa kimaksi katika kazi yake. Utafiti wake ulilenga kuibua maudhui, hata hivyo aliishilia kuhakiki vipengele mbalimbali vya mtindo kwa sababu ni vigumu kutenganisha mtindo na maudhui (Masinde, 1992).Utafiti huu ulimfaa mtafiti kuelewa dhana ya maudhui katika kazi za fasihi kwani maudhui ni mawazo makuu ya msanii kuhusu jamii inayomzunguka.

King’ei (2012), Kwenye tahakiki ya Mstahiki Meya ameelezea muhtasari wa maonyesho, uhusika, maudhui, dhamira, na mtindo wa tamthilia ya tamthilia Mstahiki Meya. Hata hivyo, tahakiki yake ni ya kijumla na inalenga kuwaongoza watahiniwa wa shule za upili kujiandaa kwa mitihani ya fasihi madhali tamthilia hii ni mojawapo ya vitabu teule.Tahakiki ya King’ei ilisaidia kuongoza utafiti huu kuunda hojaji za walimu na wanafunzi kuhusu uelewa na ufaafu wa maudhui katika tamthilia wanazosoma shuuleni na zaidi kujua iwapo Maudhui ya kazi za fasihi hususan tamthilia yanalenga hali halisi katika jamii.

Okwena (2013) ametafitia matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu teule za Arege. Amechanganua aina mbalimbali za jazanda alizotumia mwandishi huyu kuwasilisha maudhui yake.Msanii yeyote wa kifasihii hutumia mbinu kuwasilisha maudhui yake kama anavyoyaona au kuhisi katika jamii yake.Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwa mtafiti kwani ulimsaidia kuelewa Maudhui kupitia kwa uwasilishaji wa kijazanda.Okwena pia aliupa mwangaza utafiti hii kwa kumsaidia mtafiti kuelewa tamthilia za Arege kwa mojawapo wa tamthilia teule za utafiti huu,Mstahiki Meya (2009) ni kazi yake

Mwita (1994) amehakiki mbinu za sanaa zilizotumiwa kusuka maudhui ya tamthilia mbili za Ebrahim Hussein: Arusi na Ukingo wa Thim. Mwita amechambua mbinu hizi katika muktadha wa maudhui yanayowasilishwa katika tamthilia hizi akiongozwa na Nadharia ya Mtindo. Yeye anaonekana kuyapa maudhui uzito katika maelezo ya tasnifu yake. Utafiti wa Mwita kuhusu maudhui uliupa utafiti huu msingi wa kuelewa Maudhui ya tamthilia wa wasanii wawili tofauti Arege .T (2009) na Kea .P (2016) na kuyalinganisha na maudhui halisi katika jamii ya leo .

Mwanakombo (1994) amehusisha falsafa na dhamira katika uhakiki wake wa mtindo katika tamthilia za Chacha N. C,akionyesha namna zinavyoathiri mitindo ya mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wake. Mwanakombo (keshatajwa) alitathmini athari ya falsafa na dhamira kwa mtindo ilhali utafiti huu umeshughulikia vipengele vya mtindo na athari yao kwenye maudhui katika tamthilia teule. Utafiti huu kimsingi umeshughulika mtindo kama kipengele muhimu kinachoamua uelewekaji wa maudhui.Kwa kutumia utafiti huu uliolenga msingi wa kimtindo kuwasilisha maudhui mtafiti alisaidika kujua namna ya kutambua maudhui akiongozwa na mtindo na kisha kuyachunguza maudhui makuu pekee kwa msingi wa uhalisia wake.

Ongarora (2007) alishughulikia Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine. Mtafiti huyu ameshughulikia mtindo katika uwasilishaji wa maudhui akiongozwa na nadharia ya kimtindo. Tofauti ni kuwa utafiti ulishughulikia kipera cha hadithi fupi ilhali sisi tumeshughulikia tamthilia. Hata hivyo tafiti zao zitasaidia katika maelezo ya maana ya mtindo na vipengele vyake na jinsi vinavyosaidia kukuza maudhui katika utafiti huu wa kuyatathmini katika tamthilia teule.

Kwa upande mwingine, Fadhili (2014) amechunguza dhima ya mtindo katika tamthilia za kihistoria. Fadhili amelinganisha tamthilia ya Morani na Kinjekitile kwa mkabala wa Muthoni (2014) kuhakiki mtindo na maudhui katika riwaya ya Tikitimaji ya Wamitila. Muthoni amechunguza maudhui na matumizi ya lugha katika riwaya hii na kubainisha kuwa ujumbe wa mwandishi hueleweka kwa utegemezi wa mbinu za lugha alizotumia.

Maoni haya yaliyotolewa na wataalamu na wahakiki mbalimbali katika tafiti zao yataupa utafiti wetu maelezo kuhusu nadharia ya uhalisia na vipengele mbalimbali vya kutathimini maudhui katika tamthilia teule za *kigogo na mstahiki meya.*Maudhui hayo ni pamoja na ukoloni mamboleo,ufisadi,umasikini,uchafuzi wa mazingira,kupanda kwa gharama ya maisha,tamaa na ubinafsi na ukiukaji wa haki za kibinadamu.

**Nadharia ya uhalisia.**

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia hii iliasisiwa katika karne ya kumi na tisa na kufafanuliwa zaidi na E. Goffman (1952) anayeishi kati ya mwaka (1922- 1982). Baadhi ya wataalamu wengine wanaotoa mchango wao ni Gustav Flaubert (1850), George Lukacs (1979), Rene Wellek (1960), Macdowell Arthur (1918) na Hegel G. (1971). Lukas (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa na njia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Mwandishi anapaswa kupenya chini ya picha za kijuujuu na kudhihirisha mifanyiko ya mabadiliko yaliyopo. Uhalisia wa maisha katika jamii unapewa msingi mkubwa wa uandishi kuhusu uhalisia. Tukio, mhusika au mandhari huelezwa kama vya kihalisia ikiwa vinafanana na sura fulani ya maisha.

Naye Wamitila (2002) anaeleza kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Waaandishi wa kazi ya teule wanatoa picha za wahusika, matukio na mandhari ambayo yanaoona kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii. Hivyo basi, lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi ambayo ni zao la jamii. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa iwakilishe ukweli na kuwakilishwa kwa maneno halisi, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira.

Kulingana na Mwenda Ntarangwi (2004), nadharia hii katika upana wake, humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa kwa sababu za kupinga mkondo wa ulimbwende. Mhalisia huamini katika matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Vile vile, wahalisia huiamini demokrasia kama hali ya maisha, na malighafi anayochagua kueleza maisha ni yale ya kawaida, ya kadiri na ya kila siku. Hivyo basi uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi na matokeo yanayoweza kuthibitika.

Imani ya mhalisia ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli, na halisi. Hivyo basi hata picha za ulimwengu atakazoumba msanii, zapaswa kudhihirisa hali hiyo. Kama tulivyotaja hapo juu, uhalisia ulizuka ili kupinga ulimbwende ambao ulizingatia mambo ya kihisia na halisi maishani.

Wahalisia wanaona kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwa sahihi, iliyo wazi na inayozingatia maswala halisi moja kwa moja bila kupiga chuku. Maswala ya kati maishani huhusu maadili na hivyo basi msanii hana budi kuyazingatia kwa kiwango fulani cha uteuzi. Wahalisia wanashikilia kwamba msanii anapaswa kuteua lakini akiwa na nia ya kuendeleza maswala yake kama yanavyowahusu watu katika hali halisi za maisha. Mwelekeo huu wa uhalisi katika utunzi unamfanya mhalisia kumwona mhusika kama kiungo muhimu sana katika kazi ya fasihi. Hivyo basi anazingatia saikolojia ya wahusika katika hadithi.

Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia, hupembua namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia na wahusika aliowasawiri. Hivyo basi, mhakiki hutizama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalum.

Kwa muhtasari basi msanii anatarajiwa kusawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati wake. Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kihalisia. Shida inayoletwa na nadharia hii ni kuchukulia kwamba uhalisi na maana yake hauna utata wowote katika jamii yoyote, ni kwamba unachukulia kuwa watu wote katika jamii hiyo waona uhalisi mmoja na kuwa na fasili sawa kuhusu maisha yao.

Katika utafiti huu kwa kutumia tamthilia teule tutajaribu kutathmini wa maudhui katika tamthilia teule za kutahiniwa katika shule za upili na ufaafu wa maudhui hayo kwa kuyalinganisha na kuyalinganua

**Misingi Ya Kinadharia**

1. Kazi ya fasihi inajitosheleza. Tamthilia ni kazi ya sanaa kwa vile ina msuko, mtindo, wahusika na ujumbe. Mhimili huu unatusaidia kuonyesha kuwa tamthilia teule ni kazi ambazo zinajitosheleza kama kazi ya fasihi. Hii ni kwa sababu zina sura, ploti, maudhui, wahusika na zinatumia mitindo ya kisanii.
2. Kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira yake. Uhalisia sharti ujihusishe na mambo halisi yanayotokea katika mazingira halisi kupitia kwa wahusika. Mhimili huu unatusaidia katika uchanganuzi wa masuala ibuka katika riwaya za kisasa yaliyo ya kikweli katika jamii ya sasa.
3. Wahusika ni vielelezo yakini vya binadamu wa kawaida kwa vile wao hutumia lugha ya binadamu wa kawaida. Hali halisi ya ya wahusika na lugha wanayoitumia humwezesha mwanadamu kujifafanulia uwezo wake wa kutenda mambo na mtazamo wake kuhusu maisha. Mhimili huu unatumiwa kuonyesha kuwa wahusika wa tamthilia teule wanaathiriwa na yale wanayoyapitia.
4. Msanii anaangalia matatizo na kuchunguza chanzo chake. Anachunguza mabadiliko ambayo hutokea kwa kipindi fulani cha historia na kuyatumia kuwasawiri wahusika wake. Mhimili huu unatumiwa kuonyesha kuwa matatizo wanayoyapitia wahusika wa tamthilia teule yana chanzo chake

**Eneo la utafiti na uteuzi wa sampuli.**


Utafiti huu ni wa kifasihi na utajihusisha na utanzu wa tamthilia. Tamthila zilizoteuliwa *Mstahiki Meya( Arege 2013) na ile ya Kigogo( Kea 2018)*ni za Kiswahili na ambazo zimeteuliwa tutahiniwa kati ya mwaka 2013 na 2021. Tamthilia teule zitasomwa na maudhui kuchanganuliwa ili kutathmini mchango wake kwa wanafunzi wa shule za upili ambao watatumika kiwakilisha jamii.

Eneo la utafiti huu ni maktabani na sababu za kuchagua eneo hili ni upatikanaji wa maandishi.Pia utafiti nyanjani. Shule za upili katika kata ndogo ya Nzambani kauti ya Kitui zitatumika kukusanya data kutumia hojaji. Sababu ya kuchangua eneo hili ni kwa sababu ya ukaribu wake na mtafiti na pia kwa sababu eneo hili linatumika kupata picha ya jamii kwa jumla kwa kuwahoji vijana na wasichana katika shule kumi na sita za vijana na wasichana na zile mseto ili kuwakilisha jamii . Utafiti pia utafanywa mtandaoni kupata maoni zaidi ya waandishi na watafiti wengine.
Tamthilia tatu zilizoteuliwa ni kazi za Arege zilizochapishwa *Mstahiki Meya (2009*) na *kigogo (2016*). Utafiti pia utalenga wanafunzi na walimu wa shule za upili ambao watawakilisha jamii ya leo kwani ndio wanaofunza na kutahiniwa kuhusu tamthilia teule. Shule zitakazoojiwa ni katika kata ndogo ya Nzambani kaunti ya Kitui Tamthilia zimeteuliwa kimakusudi kwa vile zina data inayohitajika kutimiza malengo ya utafiti.Tamthilia hizi zitafaa kutimiza za malengo yetu kwani kwa kutathimini maudhui yake makuu na kuyalinganua ili kubaini uhalisia wake katika jamii na kisha kuangalia masuala makuu yaliyoikumba jamii katika kipindi cha kutahiniwa kwa tamthilia hizi .

**Mielekeo ya wanafunzi kuhusu ufaafu na uhalisia wa maudhui katika tamthilia.**

Sehemu iliongozwa na lengo kuu la utafiti huu kubaini ufaafu wa maudhuimakuu katika tamthilia teule kwa wanafunzi wa shule za upili ambao hufunzwa na kutahiniwa maudhui ya kazi za fasihi zikiwemo tamthilia.wanafunzi na walimu walisampuliwa kama kiwakilishi cha jamii ili tutathimini uhalisia wa maudhui katika jamii.

**Mchoro 4.5:-**Kuonyesha Manufaa ya Maudhui ya Tamthilia





Kutoka kwa majibu yao wanafunzi themanini (80) waliosema ndio walitoa sababu kwamba maudhui yanayoendelezwa na wahusika wa kazi za tamthilia uwapa taswira za moja kwa moja za viongozi na wanajamii kwa jumla.

Zaidi walisema kuwa kupitia Kwa maudhui na tabia za wahusika wanapata maelekezo ya namna ya kuishi hata baada ya shule kwani tayari kupitia tamthilia wahisi Kama wao wanaishi katika ulimwengu halisi. Kuna idadi ya wanafunzi ishirini (20) ambao walisema maudhui ya kazi za tamthilia hayawafai baadaye. Walitoa sababu kwamba baada ya shule kidato cha nne, wao huanza ukurasa mpya wa maisha. Walisema wao hukazana kuelewa maudhui kwa lengo la kupasi mtihani tu. Kulingana nao wakitoka wanaanza hali mpya ya maisha yenye maudhui mpya kwa mjibu wa jamii. Kwa maoni yangu majibu yote yaliyotolewa ni sawa, lakini ni kweli kwamba kazi za tamthilia hasa Mstahiki Meya (2009) na Kigogo (2016) ni tamthilia ambazo zinatupa taswira ya jamii, hivyo mwanafunzi anaposoma kazi za tamthilia atakuwa na manufaa kutambua na kuoanisha mambo katika jamii baadaye.
Asilimia themanini ya wanafuzi wanaweza kutambua manufaa ya maudhui wanayosoma shuleni baadaye katika maisha yao. Walisema kuwa kupitia Kwa maudhui na tabia za wahusika wanapata maelekezo ya namna ya kuishi hata baada ya shule kwani tayari kupitia tamthilia wahisi kama wao wanaishi katika ulimwengu halisi. Kuna asilimia 20 ya wanafunzi ambao walisema maudhui ya kazi za tamthilia hayawafai baadaye. Walitoa sababu kwamba baada ya shule kidato cha nne, wao huanza ukurasa mpya wa maisha. Walisema wao hukazana kuelewa maudhui kwa lengo la kupasi mtihani tu.

**Hitimisho.**
Utafiti huu ulitafitiwa kwa kusoma tamthilia teule Mstahiki Meya (2009) na Kigogo (2016). Kutokana na kusoma na kuchambua tamthilia hizi mtafiti aliweza kulinganisha na kulinganua maudhui makuu.Kupitia kwa zoezi hili mtafiti alibaini kuwa Maudhui katika kazi za tamthilia teule ni sawa tofauti ni namna ambavyo msanii anavyotumia mbinu za lugha na wahusika wake kupitisha maudhui .utafiti huu pia ulipata data kwa kuwahoji walimu na wanafunzi katika kata ndogo ya Nzambani eneo ya kitui .

Sampuli hii ilitumiwa kuwakilisha jamii ili kubaini ufaafu wa maudhui katika tamthilia zinazoteuliwa kutahiniwa katika shule za upili na uhalisia wa maudhui hayo katika jamii.kutokana na majibu yao Idadi kubwa ya wanafuzi iliweza kutambua kuwepo kwa maudhui umaskini, ugumu wa maisha, ufisadi, ukoloni mamboleo na uongozi mbaya katika jamii.

**Mchoro 4.7**:-Kuonyesha Uhalisia wa Maudhui.




Wanafunzi tisini na tano walijibu ndio kwamba maudhui ya uongozi mbaya yapo katika jamii nao kumi wakasema la kwamba hakuna uongozi mbaya. Waliosema ndio waliweza kutetea jibu lao kwa kutoa mifano kama viongozi wengi hawajawajibika wengine wanatumia mamlaka yao vibaya kuwadhulumu wanajamii. Wanafunzi kumi waliosema hakuna uongozi mbaya walitetea kauli yao kwamba viongozi waliomamlakani si wambaya wananchi wanaowachagua ndio wambaya kwani wametaliwa na tamaa kwa hivyo wanaadaika upesi kuwachagua viongozi waovu.

Wanafunzi themanini na tano kulingana na jedwali walikubaliana na kuwepo kwa ukoloni mambo leo katika jamii ya leo.walitoa mifano ya waafrika kudhamini elimu, matibabu na lugha za kigeni kuliko zile za nchini kwao. Wanafunzi kumi na tano ambao walipinga kuwepo kwa ukoloni mambo leo walisema killichopo si ukoloni mambo leo lakini wanajamii udhamini huduma za ugenini kwa kukosa huduma bora kwao nchini.

Kulingana  jedwali wanafunzi sabini na tano walikubaliana na kuwepo kwa ufisadi katika jamii.kutona na majibu yao ni bayana kwamba ufisadi ni halisi katika jamii ukichangiwa na uongozi mbaya na tamaa na ubinafsi miongoni mwa viongozi na wanajamii. Wanafunzi ishirini na tano walielekea kutobaini hali ya ufisadi katika jamii

Kulingana na maoni ya wanafunzi kuhusu kuwepo kwa hali Kulingana na maoni ya wanafunzi kuhusu kuwepo kwa hali umaskini katika jamii. Walisema idadi kubwa ya wana jamii ni maskini wenye pato la chini. Wanafunzi 10 walisema sio watu wote katika jamii ambao ni maskini kwani kuna tabaka la juu la viongozi na matajiri ambao ndio wenye nchi. Kulingana na maoni ya wahojiwa kuhusu maudhui makuu elekezi ni wazi kuwa kuna uhalisia wa maudhui katika jamii kwa kiasi kikubwa sana.

**Marejeleo**

1. Ambrose K. Ngesa, Enock Matundura na John Kobia (2015) Mwingiliano wa matini katika tamthilia za Kiswahili: *Mashetani* na *Kijiba cha moyo.*
2. Arege, T. M. (2009). Mstahiki Meya. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.
3. Chacha, N. C. (1980). Ushairi wa Abdilatif: Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa (1971)
4. 33Chimera, R. na Njogu, K. (1999). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
5. Fridah G. O. (2017) Uhakiki Wa Mtindo Katika Tamthilia Za AregeTasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Maasai Mara. (Haijachapishwa)

6. Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2011). Toleo la pili. Nairobi: Longhorn Publishers.
7. Katutu, R. (2013). Mtindo katika Diwani ya Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
8. Kaui, T (2008) usawiri wa vijana katika tamthilia teule zaKiswahili Wakati*Ukuta* (1971) na *Uasi* (1980). Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
9. Kea, P. (2016).Kigogo.Nairobi.story Moja publishers.Ltd.
10. Kinara, G. (2012) "*Maudhui ya Ukimwi Katika Riwaya za Kiswahili*". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
11. Kitula, K. N.W. (2012). Mwongozo wa Mstahiki Meya. Nairobi: Target Publications Ltd.
12. Kothari, C. K. (1990). Research Methodology: Methods and Techniques. New Delhi: Wiley.
13. Mugambi, E. K. (1983) "*Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za Mohamed, S.A*". Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
14. Muthoni, M. (2014). Uhakiki wa Maudhui na Mtindo katika Tikitimaji. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (haichapishwa).
15. Mwanakombo, M. M. (1994). Uchambuzi wa dhamira, falsafa na mitindo katika tamthilia mbili za Chacha N. Chacha. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi (Isiyochapishwa).
16. Mwita, S. M. (1994). Tamthilia mbili za Ebrahim Hussein: Arusi na Kwenye Ukingo wa Thim. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi (haichapishwa).
17. Ng'etich, B. (2011) "Dini *kama Chombo cha Kuwadhulumu Waumini*". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
18. Ngolo, E. K. (2011). Mabadiliko ya Kimtindo katika Ushairi wa Said A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (haijochapishwa).
19. Ngonyani, D. (2005). Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake katika Jamii." Katika Swahili Forum nambari 12, Uk.122-123. Chama cha Masomo ya Kiafrika.
20. Njogu, K. (2007) *Kiswahili na Elimu Nchini*. Limuru: Kolbe Press
21. Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
22. Njoroge, A. W. (2014) "*Viongozi kama Visababishi vya Mabadiliko katika Riwaya za Mwenda Mbatiah: Vipanya vya Maabara na Majira ya Tufani".* Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).